2000

YESU alisema: Naja—

upesi

Ufunuo 22:12

“Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.”
Warumi 10:9

“Walakini usipokesha, nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.”
Ufunuo 3:3

“Tazama, Naja upesi.”
Ufunuo 22:12

“Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu.”
Mathayo 24:42

Januari/Janvier

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

Februari/Février

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29				

Marchi/Mars

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

Aprili/Avril

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
30						1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

Mei/Mai

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

Juni/Juin

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	

Julai/Juillet

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

Agosti/Août

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30	31		

Septemba/Septembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

Oktoba/Octobre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
1	2	3	4	5	6	7
8	9	10	11	12	13	14
15	16	17	18	19	20	21
22	23	24	25	26	27	28
29	30	31				

Novemba/Novembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

Desemba/Décembre

J'pili	J'tatu	J'nne	J'tano	Alh.	Ijumaa	J'mosi
31					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

Kata hapa

Jina.....No 75/.....

Anwani.....

.....

Nchi .....

KWA KUPEWA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, Andika jina na anwani yako hapa kwa HERUFI KUBWA.

Mtumie: Mr. David M. Eunson, Administrator, Bowstones, Hall Crescent, Gullane, East Lothian, EH31 2HA, Scotland, UK.

(Ukituma barua bila stampu, au ukitia stampu zisizo mpya, barua zitatupwa.)

Barua toka Congo

Barua hizi ambazo ziliandikwa na WaCongo zilitumiwa kwa rafiki zao wakaao nje ya Jamhuri Democratic ya Congo:

na Kasisi B.

"Tunawasalimieni sana katika jina takatifu la Bwana Yesu. Baada ya kuondoka kwenu tuliishi katika shida kubwa walakini Mungu ametuhifadhi. Askari waliokuwamo mjini walijaribu kusafiri kwetu lakini Mungu alinyosha mkono wake wa uwezo, nayo magaradumu ya magari yao yalichomwa njiani. Walijaribu wakiyarekebisha mchana mzima bila kufanikia. Hawakutukaribia. Hawakutuangushia bomba wala kumwua hata mmoja wetu. Mungu hutuhifadhi nasi tumtegemea sana kwa sababu Shetani anataka kutuangamiza. Ndugu zetu, tuombeeni tafadhali kwa sababu nchi yetu ina shida kubwa."

na Kasisi M.

"Tunawasalimieni katika jina takatifu la Mwokozi wetu Yesu Kristo. Twaamini ya kwamba hata kama ninyi ni mbali sana nasi, roho zenu ni karibu katika maombi. Twawakumbukeni kila tunapoomba Mungu kadhalika. Mnasikia kuhusu shida kubwa ambazo zinatudhuru nchini mwetu siku hizo. Ingawa watoto wa giza huendelea kufanya machafuko, Mungu huzidi kututia mioyo. Twaona raha mioyoni mwetu kwa sababu Mungu hututendea miujiza mingi. Kuna watu watatu walio tayari kusoma katika chuo kikuu cha Biblia lakini tunakosa pesa za kuwatuma. Twamhudumia Mungu nasi twapewa baraka zake sana.

"Juma moja baada ya kuondoka kwenu tuliomba Mungu atuunganishe kuwa kundi la waombaji. Kundi hilo lilifanywa na makasisi na wake zao, wajane, wainjilisti pamoja na wakristo kanisani na vijana wanaume kwa wanawake. Tumefurahi sana tukiona jinsi Mungu alivyojibu maombi yetu. Twaombea zaidi Wakristo wajazwe katika Roho Mtakatifu na hali kadhalika waonyeshe upendo wa Mungu kwenye majirani yao. Tafadhali wajulishe wengine watuombee."

na Daktari B.

"Namshukuru Bwana Mungu wetu kwani amenipa nafasi hiyo ya kuwasimulia kuhusu mambo yetu. Kuna kimya kwa upande wetu wa Congo ila kwa kusini ambapo wenzetu wanafichama mwituni kwa sababu ya fujo vijijini mwao. Tulipokuwa tusingalikuwamo nyumbani, wenye fujo walipitapita karibu na nyumba zetu bila kuzivamia. Twamshukuru Mungu kwa sababu hutuhifadhi katika shida hizo."

na Kasisi A.

"Jamaa yangu wanaungana nami kwa kuwasalimu katika Kristo. Tulikuwa tumekaa mwituni mpaka mwezi wa Oktoba naye Bwana alituhifadhi. Tukawaona askari wengi njiani ambao walikimbia na wengine waliokuwa wakipigana, walakini hawakumdhuru binti yangu. Mungu asifiwe."

Watu wawili walinitembelea

na Adeli Aduiri, Pwani ya Pembe

Ingawa babangu alikuwa mchungaji wa kanisa fulani, mimi sikuwahi kumwamini Mungu. Hata hivyo nilipewa neema ya Bwana akinitumia watu wawili ili wanizungumzie kuhusu habari za Yesu. Nikaanza kwenda kanisani. Hapo nilijitambua ya kwamba nilikuwa mwenye dhambi. Nikamsihi Bwana anisamehe naye alinisikia. Siku moja baadaye nilipewa gazeti la UPESI nikalisoma.

Baada ya muda mdogo niliacha kwenda shuleni kwa kuwa nilifanya makosa nami nimeolewa isivyo halali. Kwa hiyo hata magazeti nikawa nayo sikuyasoma tena. Baadaye nilivutwa sana katika fikira zangu kuhusu zile shuhuda ambazo nilikuwa nimezisoma. Ndipo nikaanza tena kuyasoma magazeti ya UPESI na pia nikatiwa moyo kuisoma Biblia. Neno lake Mungu lasema, **"...yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? ...Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."** (Matendo 16:30, 31)

Bwana Yesu hunihifadhi kwani aliniponya kwa ugonjwa hatari wa kipindupindu na homa nguvu kadhalika. Yesu hunitendea mambo mengi sana. Namshukuru Bwana kwa mambo yote aliyonitendea pia. Namsihi awatie nguvu wote wanaomfikilia.

Feba Radio Broadcast Schedule

Time UTC/GMT	Language	Frequencies (kHz)
0315-0400 (Su, Mo, We, Th, Sa)	SWAHILI	11750
0315-0345 (Tu, Fr)	SWAHILI	11750
1615-1700 (Su, Mo, Tu, We, Fr, Sa)	SWAHILI	11745
1615-1700 (Th)	SWAHILI	11745

Zaburi 139

Ee BWANA, umenichunguza na kunijua.
Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu;
Umelifahamu wazo langu tokea mbali.
Umepepeta kwenda kwangu na kulala kwangu,
Umeelewa na njia zangu zote.
Maana hamna neno ulimini mwangu
Usilolijua kabisa, BWANA.
Umenizingira nyuma na mbele,
Ukaniwekea mkono wako.
Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi,
Hayadirikiki, siwezi kuyafikia.
Niende wapi nijiepushe na roho yako?
Niende wapi niukimbie uso wako?
Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko;
Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko.
Ningezitwaa mbawa za asubuhi,
Na kukaa pande za mwisho za bahari;
Huko nako mkono wako utaniongoza,
Na mkono wako wa kuume utanishika.
Kama nikisema, Hakika giza litanifunika,
Na nuru inizungukayo ingekuwa usiku;
Giza nalo halikufichi kitu,
Bali usiku huangaza kama mchana;
Giza na mwanga kwako ni sawasawa.
Maana Wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu,
Uliniunga tumboni mwa mama yangu.
Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa
Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha.
Matendo yako ni ya ajabu,
Na nafsi yangu yajua sana,
Mifupa yangu haikusitirika kwako,
Nilipoumbwa kwa siri,
Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi;
Macho yako yaliniona kabla sijakamilika;
Chuoni mwako ziliandikwa zote pia,
Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.
Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu;
Jinsi ilivyo kuwa jumla yake!
Kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga;
Niamkapo nikali pamoja nawe.
Ee Mungu, laiti ungewafisha waovu!
Enyi watu wa damu, ondokeni kwangu;
Kwa maana wakuasi kwa ubaya,
Adui zako wakutaja jina lako bure.
Je! BWANA nisiwachukie wanaokuchukia?
Nisikirihike nao wakuasio?
Nawachukia kwa ukomo wa chuki,
Wamekuwa adui kwangu.
Ee Mungu, unichunguze, uujue moyo wangu,
Unijaribu, uyajue mawazo yangu;
Uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu,
Ukaniongoze, katika njia ya milele.

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina lako na anwani yako kwa:

Katika KENYA: Evangel Bible Courses, SLP 28963, Nairobi, Kenya.

Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Jam. Dem. ya Congo.

Katika TANZANIA: Emmaus Bible School, SLP 9322, Dar-es-Salaam, Tanzania.

TANGAZO

Kwa wasomaji katika Tanzania:
Sanduku la posta kwa Tanzania limefungwa. Tafadhali tumie anwani ya Mr. David Eunson kwa kupewa nakala ya UPESI.
Ukitaka kusoma UPESI kwa INTERNET, tumie
http://soon.org.uk/upesi